

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Januari, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika mwezi huu wa Januari, tumepata misiba mitatu kwa mfululizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro kupitia Chama cha CHADEMA, alifariki dunia tarehe 14 Januari, 2012 kufuatia ajali ya gari iliyotokea eneo la Ruvu, Mkoani Pwani. Mazishi yalifanyika tarehe 18 Januari, 2012 kijijini kwake Ifakara, Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, alifariki dunia tarehe 19 Januari, 2012 katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili. Mazishi yalifanyika tarehe 23 Januari, 2012 Kijijini Akeri, Arumeru, Mkoani Arusha.

Aliyekuwa Mtumishi wa Bunge katika Kitengo cha Ugavi, Ndugu Nicodemus Luther Senge, alifariki dunia tarehe 21 Januari, 2012 kwa kupigwa risasi katika ugomvi wa kifamilia. Mazishi yalifanyika tarehe 24 Januari, 2012 Mkoani Arusha. Waheshimiwa Wabunge, naomba tusimame kwa dakika moja ili kuziombea roho za Marehemu hao.

(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuomboleza vifo tajwa hapo juu)

Kwa mujibu wa Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, katika Mkutano wa Tano wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali ifuatayo; Muswada wa kwanza ni *Public Procurement Bill, 2011* na Muswada wa pili ni *The Constitutional Review Bill, 2012*. Mara baada ya kupitishwa na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Miswada hiyo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili ipate kibali chake. Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, Miswada hiyo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa sheria za nchi zinazoitwa *The Public Procurement Act, No. 7, 2011* na *Constitutional Review Act (No. 8) 2011*. Mwisho wa taarifa.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Tano wa Bunge uliopita.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir.

Na. 1

Tatizo la Dawaa za Kulevya

MHE. KHERI KHATIB AMEIR aliuliza:-

Suala la mihadarati na dawaa za kulevya ni tatizo kubwa nchini, linapoteza nguvu kazi na maliasili nyingi:-

- (a) Je, nini ukubwa wa tatizo hilo Kitaifa na mipango ya kukabiliana nalo?
- (b) Je, kwa kipindi cha miaka mitatu nyuma ni kiasi gani cha dawaa za kulevya kimekamatwa na hatua gani zimechukuliwa kwa wahusika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?
- (c) Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Dirisha la Mawasiliano kwa kutoa namba za simu zitakazoweza raia wema kuwasiliana na kutoa taarifa za waingizaji wakubwa wa dawaa hizo nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mbunge wa Matemwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali inatambua kuwa tatizo la matumizi na biashara haramu ya dawaa za kulevya nchini ni kubwa. Ukubwa wa tatizo hili unadhihirishwa na takwimu zilizokusanywa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 – 2010 ambazo zinaonesha kiasi cha dawaa za kulevya kilichokamatwa na idadi ya watuhumiwa kama ifuatavyo:-

Bangi tani 2,953.3 zilikamatwa na watuhumiwa waliokamatwa walikuwa 51,266.7 Mirungi tani 68.5 zilikamatwa na watuhumiwa walikuwa 4,000. Heroin kilo 607.4 zilikamatwa na watuhumiwa walikuwa 2,473 na Cocaine ni kilo 120 na watuhumiwa waliokamatwa ni 932.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mipango na mikakati ya kukabiliana na biashara na matumizi ya dawaa za kulevya nchini kupitia vyombo mbalimbali vya Serikali ambavyo baadhi yake ni Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa na vingine vyote vinavyohusika, ambavyo kwa majibu ya karatasi niliyonayo, nitamkabidhi Mheshimiwa muuliza swali kwa sababu orodha ya taasisi zinazoshughulikia jambo hili ndefu.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kuimarisha zoezi na kuzuia na kupambana na dawaa za kulevya, Serikali imekwishaanza mchakato wa kutunga Sera ya Taifa ya Kudhibiti Dawaa za Kulevya na Sheria Mpya ya Kuzuia na Kupambana na Dawaa za Kulevya, ambazo zinapendekeza kuundwa kwa chombo kipya kitakachoitwa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawaa za Kulevya.

- (b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu (2009 – 2011), kwa upande wa Tanzania Bara, dawaa za kulevya zilizokamatwa ni kama ifuatavyo: Bangi tani 75.5, Mirungi tani 26.7, Heroin kilo 458.14, Cocaine kilo 193.69, Mandrax kilo 0.9 na Morphine kilo 2.12. Zoezi la ukamataji limeonesha mafanikio mazuri sana miaka ya hivi karibuni, ambapo kuanzia mwaka 2010 hadi Machi, 2011 jumla ya kilo 443.6 za Heroin zilikamatwa kati ya kilo 607 zilizokamatwa kwa kipindi cha mwaka 2000 hadi 2010. Aidha, katika tukio moja tu la mwezi Machi 2011,

kiasi cha kilo 81 za Cocaine kilikamatwa. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, dawa zilizokamatwa katika kipindi cha mwaka 2009 – 2011 ni kama ifuatavyo: Bangi tani 0.055, Heroin kilo 1,432 na Cocaine kilo 0.717.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha miaka mitatu (2009 – 2011), jumla ya watuhumiwa 35,870 walikamatwa na kufunguliwa kesi. Watuhumiwa walioitiwa hatiani ni 35,746, watuhumiwa watano waliachiwa huru na kesi 192 bado zinaendelea kusikilizwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania.

(c) Mheshimiwa Spika, tayari Jeshi la Polisi limetoa namba za simu kwa Wananchi ili watoe taarifa wanapohisi watu fulani wanajihusisha na vitendo vya uhalifu ikiwemo biashara haramu ya dawa za kulevya. Wazo la kuanzisha Dirisha la Mawasiliano ya Simu kwa vyombo vyote ni zuri, Serikali itaifanyia kazi. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana Wananchi kwa taarifa wanazotupa na kuwaomba waendeleo kushirikiana na Serikali kwani tatizo hili linagusa maisha ya Watanzania wote.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Watanzania tuna tabia, naweza kusema kwamba siku zote huwa tunasema tunaunda vyombo:-

- (i) Katika jibu lako hili chombo hiki kitaundwa lini; lini tutakijua; na lini kitaanza kufanya kazi?
- (ii) Mheshimiwa Rais wakati fulani alipotembelea Mikoa ya Kusini alitoa tamko kwamba kuna baadhi ya wanadini wanajishughulisha na masuala haya. Hili suala limefikia mahali gani na hawa watu wamechukuliwa hatua gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mbunge wa Matemwe, kama ifuatavyo:-

Tulipofanya semina hapa ya Waheshimiwa Wabunge, tulieleza umuhimu wa kuunda chombo kimoja chenye nguvu, kwa sababu shughuli hizi sasa zinashughulikiwa na vyombo vingi. Kwa mfano; Tume ya Kuratibu Shughuli za Dawa za Kulevya ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Polisi pia wana Kitengo cha Dawa za Kulevya na idara mbalimbali nazo zinashughulikia masuala haya. Kwa hiyo, tunafikiri ni lazima kuwe na chombo kimoja ambacho kitakuwa na wataalam wote wanaohusika, ambao watakuwa na uwezo wa kukamata na kushtaki na kushughulikia wale vijana ambao wamepatwa na matatizo hayo kwa pamoja. Kwa hiyo, hicho chombo sasa hivi tumekitungia Sera na Sheria.

Nataka kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, vyombo hivi vyote na maandishi yote yameshafikia kwenye ngazi ya juu sana na ni nia yetu Serikali kwamba, tutaharakisha hili jambo ili liwe wazi. Tuligundua siku ile wakati wa semina kwamba hata sheria nyingine zinakinzana kiasi kwamba hata watoa haki hawatoi haki za msingi kulingana na makosa yalivyo. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna umuhimu katika jambo hili, kurekebisha sheria, kutunga Sheria na Sera. Kwa hiyo, hilo jambo tunalifanya.

Juu ya Viongozi wa Dini; wakati wa Semina tulitoa mfano wa Kiongozi mmoja ambaye ameshakamatwa na kesi yake ipo Mahakamani, lakini vitendo hivi vimekuwa vinajitokeza tokeza na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, alitoa rai wakati ule akiwa Mikoa ya Kusini. Wale wote ambao wamejihusisha na jambo hili, wawe ni Viongozi wa Dini, wafanyabiashara au watu wa kada zote, kesi zao ziko Mahakamani na wengine kesi zao zimeamriwa. Kuhusu hawa Viongozi wa Dini waliohusika, kesi zao ziko Mahakamani na siku ile wakati wa semina Waheshimiwa Wabunge, tuliwaonesha hata picha ya mhusika.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Katika makundi haya ya dawa za kulevya ambazo Serikali imezorodhesha kwa mikoa mingine kwao ni mboga au ni dawa:-

Je, watuhumiwa wa mikoa hii wakikamatwa adhabu yao ni ile ile ya mtu ambaye amekamatwa na heroin?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, kama ifuatavyo:-

Sina ushahidi kama kuna sehemu nyingine dawa za kulevya ni mboga, labda Mheshimiwa Spika anajua kama kuna sehemu watu wanafanya mboga dawa za kulevya. Hizi ni habari za kusikika kwamba, bangi sehemu nyingine ni mboga. Sasa labda tuulizane, mimi sijawahi kupata ushahidi huo, wenye ushahidi watuambie. Tunajua kwamba, bangi imeharamishwa na kwa mujibu wa sheria, bangi ni miongoni mwa dawa za kulevya. Kwa hiyo, mtu yeyote anayelima, kuvuta au kufanya biashara ya dawa hizi, anavunja sheria kwa mujibu wa sheria zetu za nchi.

SPIKA: Siyo mboga wala siyo nini, maana yeye anaizungumzia Njombe, ilishafutwa zamani lakini siyo mboga ilikuwa viungo. *(Kicheko)*

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kule Zanzibar Mbwa wa Polisi anayetumika kuchunguza dawa za kulevya amefariki dunia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mbwa mwingine haraka iwezekanavyo kabla wahalifu hawajatumia huo mwanaya? *(Makofi)*

SPIKA: Haya, mimi sijui kama Mheshimiwa Waziri alijiandaa na swali la Mbwa aliyefariki. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, nadhani unawajua Mbwa wako wote? *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kwamba, Chombo cha Polisi kitaendelea daima wala siyo kwamba ni mtu binafsi isipokuwa ni taasisi iliyokamilika. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tumeondokewa na huyo Polisi, lakini kazi zinaendelea na wapo Polisi wengine watawekwa kutazama majukumu haya.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inaonesha kuwa na jitihada maalum za kuwazuia wanaofanya biashara ya dawa za kulevya:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kujenga Maeneo Maalum *(Rehabilitation Centres)* ili kuwapa huduma na kuwapunguzia mzigo vijana wengi walioathirika na dawa hizi kama nchi nyingine zinavyofanya; na vilevile ili kupunguza wale watu ambao wanaleta dawa kutokuwa na wateja wengi katika nchi yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inavyo hivyo vituo lakini kulingana na uzoefu tulionao, vituo hivi vimekuwa haviendeshwi vizuri sana. Tunajua tunavyo vituo katika Serikali ya Muungano na kimojawapo kipo hapa Milembe, lakini Zanzibar nao wana vituo vyao na watu binafsi wamejitolea kuanzisha vituo vya namna hii vya hiari na wanafanya vizuri sana. Kutokana na matatizo ya uendeshaji wa vituo hivi, ndiyo maana tumeamua sasa tuweke Sera na Sheria ambayo itakuwa na chombo kimoja kitakachokuwa kinafanya shughuli zote pamoja na shughuli hii ya uragibishi kwa vijana hawa ambao wametumia dawa za kulevya. Kwa hiyo, tunavyo hivi sasa lakini tutaviimarisha kupitia chombo hiki kipiya ambacho kitaundwa.

Tatizo la Madawati Nchini

MHE. VINCENT J. NYERERE aliluliza:-

Je, Serikali imejipanga je kumaliza tatizo la madawati nchini kwa kuwa kuna upungufu mkubwa na misitu ya mbaao ipo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwepo wa madawati ni sehemu ya vigezo vya kuwepo mazingira bora ya kufundishia na kujifunza shuleni. Mahitaji ya madawati hutegemea idadi ya wanafunzi waliopo shuleni. Aidha, ni wazi kuwa dawati ni kifaa muhimu kwa mwanafunzi akiwa shuleni ili kuongeza ufanisi wake wa kujifunza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari, umekwenda sambamba na idadi ya wanafunzi walioandikishwa shuleni kuongezeka kwa kasi. Hali hiyo imeongeza pia uhitaji wa ongezeko la madawati. Serikali kupitia Halmashauri nchini, imekuwa ikielekeza utaratibu wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo mikakati ya kupunguza tatizo la madawati kwa wanafunzi mashuleni pamoja na kuhusisha pia wadau mbalimbali katika kupunguza upungufu wa madawati. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Serikali ilitoa fedha kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa madawati kwa Shule za Sekondari na mwaka 2010/2011, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni tatu kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ununuzi wa madawati kwa Shule za Msingi. Kwa upande mwingine, Viongozi wa Shule wamekuwa wakisisitizwa kutumia kifungu cha ukarabati, kufanya matengenezo kwa madawati yote mabovu yaliyopo shuleni ili kuondokana na hali ya upungufu uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa misitu, lakini Serikali imetoa fursa ya kuvuna miti kwa kufuata taratibu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo utengenezaji wa madawati. Halmashauri zote zina maelekezo ya uvunaji endelevu wa misitu iliyopo.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali ipo tayari kutupatia vibali Wabunge ambao tuna upungufu wa madawati vya kupasua mbaao kwa ajili ya kutengeneza madawati hayo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, Serikali imetoa nafasi ya kuvuna misitu kwa kufuata utaratibu katika kila Halmashauri na kwamba Halmashauri zote zimepewa maelekezo hayo na upo utaratibu ulioandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; kwa kuwa tatizo hili la madawati ni kubwa sana; na kwa kuwa kuna fedha za rada ambazo tulisikia kwamba zitaelekezwa pia upande wa elimu katika Shule za Msingi kwenye upande wa vitabu na madawati; je, Wizara ipo tayari kutatua tatizo hili kwa kutoa tenda kwa taasisi zetu kama Magereza, JKT au VETA? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwenye utaratibu wa *bio-system*, fedha ambazo Mheshimiwa Mlata ametaka kujua, katika fedha zile tumetengewa shilingi 18,400,015,000 ambazo pia zitaingia katika Mpango wa Utengenezaji wa Madawati kwa Shule za Msingi na ndiyo hasa uliopewa kipaumbele.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, lakini swali nililotaka kuuliza limeshaulizwa.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa suala la upungufu wa madawati huko nyuma Serikali ya Chama cha Mapinduzi imewahi kulichukulia ufumbuzi ambao ulionyesha tija kubwa sana na kumaliza tatizo la upungufu huo; na kwa kuwa wajibu wa mipango ya kumaliza tatizo hili kwa kweli hasa ni la Halmashauri zetu na hatua ipo hivyo na hali ipo hivyo hivi sasa. Je, Serikali Kuu inasema nini juu ya suala zima la kumaliza tatizo hili kwa sababu hali ya upungufu wa madawati siyo nzuri?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ni kweli shule zetu za Sekondari na Msingi zina uhaba wa madawati. Mwaka huu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeandaa Waraka ambao hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu ataupeleka katika Halmashauri zote kutangaza kwamba huu ni mwaka wa kumaliza matatizo ya madawati.

Tutamaliza tatizo hili; kwanza, kama kawaida kutokana na fedha kidogo tunazopata kutoka Serikalini kwenye bajeti. Pili, kama ilivyowahi kudokezwa, Wizara ya Fedha imetuhidi kwamba itatupatia fedha za kutatua matatizo ya elimu na sisi kwa sababu tumedhamiria mwaka huu kuwa ni mwaka wa kumaliza matatizo ya madawati, tumedhamiria fedha zile kiasi kikubwa tupeleke katika kuondoa tatizo la madawati.

Mwisho, nataka kumalizia kwa kusema kwamba, Shule za Msingi ni mali ya Serikali za Vijiji, Shule za Kata ni mali ya Kamati za Maendeleo za Kata, bado pamoja na jitihada hizo za Serikali hatutaweza kumaliza tatizo hili bila kushirikisha nguvu za Wananchi. Sera ya Serikali ya CCM ni kuchanganya nguvu za Wananchi pamoja na jitihada ya Serikali katika kuondoa matatizo; na kwa hiyo, napenda kutoa mwito kwa Wananchi wote wa Tanzania, tushirikiane na Serikali yetu tushiriki kutoa michango ili kuziba pengo ambalo halitaweza kutekelezwa kwa jitihada za Serikali peke yake.

SPIKA: Ahsante. Hasa kujenga choo ni lazima Wananchi wajenge siyo Serikali.

Na. 3

Fursa ya Wanawake Kutoa Maoni Yao Juu ya Katiba Mpya

MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. AMINA N. MAKILAGI) aliluliza:-

Wakati Serikali ikijiandaa kuelekea kukusanya maoni ya Wananchi juu ya kupata Katiba Mpya, zipo baadhi ya jamii za Kitanzania wasiopenda kuona/kusikia wanawake wakizungumza mbele ya jamii kutoa maoni yao:-

Je, Serikali imejiandaa je kuhakikisha kuwa wanawake wanawekewa mazingira mazuri ya kuwawezesha kutoa maoni yao kwa uhuru na uwazi kuziondoa sheria zote zinazowadhilisha wanawake na watoto ili zisiingie katika Katiba Mpya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali, napenda kutoa maelezo mafupi kwamba, tangu tulipopata Uhuru wa Tanzania Bara, tarehe 9 Desemba 1961, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika juhudi za kumkomboa mwanamke na kulinda haki za mtoto. Tanzania vilevile imeridhia Mikataba ya Kimataifa inayotetea Mwanamke na Mtoto. Mkataba unaotetea Haki za Mwanamke (*Convention on Elimination against Women*), uliridhiwa mwaka 1985 na Mkataba unaotetea Haki za Mtoto (*Convention on the Rights of the Child*), uliridhiwa mwaka 1991.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ibara ya 66(1)(b), inatoa nafasi kwa wanawake kupata nafasi maalum ya kuwawakilisha Wananchi katika Bunge letu. Zipo pia sheria ambazo zimefanyiwa marekebisha ili ziweze kumlinda mwanamke na mtoto. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009. Hayo ni baadhi tu ya mambo machache kati ya mengi ambayo Serikali imeyafanya katika kutetea haki za wanawake na watoto nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Wananchi wote nchini bila kujali jinsia, rangi ya mwili au uwezo wa kifedha, wataelimishwa kuhusu Katiba ya sasa, haki yao ya kutoa mawazo na kuheshimu maoni ayatoayo kila mmoja. Ibara ya 18 ya Katiba niliyoitaja hapo juu, inaeleza uhuru wa kutoa maoni kwa kila Mtanzania. Ibara hiyo inaeleza kama ifuatavyo:-

Kila mtu-

- (a) anao uhuru wa kuwa na maoni ya kueleza fikra zake;
- (b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;
- (c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na
- (d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za Wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa Wananchi wote wanaelimishwa kuhusu Katiba ya sasa na pia kuhakikisha wanapata fursa sawa ya kutoa maoni yao kwa ajili ya kutungwa kwa Katiba Mpya. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na kuandaa mikutano ya hadhara, vipindi vya radio, TV, magazeti na Makongamano. Aidha, Wizara inayo tovuti yake (www.sheria.go.tz), ambayo inaweza kutumika kupokea maoni juu ya Katiba Mpya. Mtu au watu watakaobainika kuwazuia watu kutoa maoni yao kwa sababu yoyote ile, watakuwa wametenda kosa la jinai na sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya jamii wasiopenda kuona au kusikia wanawake wakizungumza mbele ya jamii na kutoa maoni yao, Tume itaweka utaratibu utakaohakikisha makundi hayo yanafikiwa. Itakuwa ni jukumu la Tume kuwasiliana na Halmashauri za Wilaya ili pale penye matatizo hayo, utaratibu mzuri wa kuyafikia makundi hayo uweze kuandaliwa. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sote tuwe katika mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Watanzania wote wenye uwezo wa kutoa maoni yao wanapata fursa hiyo ili tuweze kupata Katiba nzuri itakayokuwa imeshirikisha Wananchi wengi.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kuna baadhi ya watu au makundi ya watu wameamua kuwapotosha Wananchi kwamba muda utakapofika wa kutoa maoni watakatwa na wala hawataruhusiwa kutoa maoni na wengine watafungwa kwa sababu ya kutoa maoni na wameanza kazi hiyo kabla ya Tume kuanza kazi kuwapotosha Wananchi. Je, Serikali inawachukulia hatua gani watu kama hao ambao wameanza kuwapotosha Wananchi wasiojua kinachoendelea?

(ii) Kwa kuwa Wananchi wengi wanalalamika kwamba hawana Katiba ya zamani ambayo inatakiwa kufanyiwa marekebisha; Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wanapata Katiba hizo na kuzisoma kabla ya kuanza kutoa maoni yao? (Makofi)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, suala la upotoshaji wa jamii huwa linatokea, lakini ni wajibu wetu sisi kama Viongozi hasa Wabunge

kuwaeleza ukweli juu ya jambo hili. Naamini kwamba, Wabunge kupitia Majimbo katika maeneo yetu, tukiweza kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa wao kutoa maoni, upotoshaji unaofanywa na watu wachache hautakuwa na madhara makubwa. Hata hivyo, sheria iliyopo wakati mchakato utakapoanza inalinda nafasi ya Tume katika kupokea maoni. Kwa yeyote atakayedhihirika kwamba anafanya upotoshaji kwa nia ya kuizua Tume kupata maoni, vile vile sheria itafuata mkondo wake.

Kuhusu suala la kushirikisha elimu ya Katiba ya sasa, Wizara ya Katiba na Sheria inaandaa vipeperushi, inachapisha hivi sasa nakala za Katiba iliyopo kusambaza hii elimu ili kuwafikia watu wengi zaidi ili waweze kujua na hivyo kuwapa fursa zaidi ya kuweza kutoa maoni wakiwa wanajua Katiba ya sasa inasema nini na maoni yao yapi.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nashukuru swali langu ambalo nilitaka kuuliza Mheshimiwa Waziri amelijibu vizuri sana la kusambaza Katiba kwa Wananchi.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameorodhesha itifaki na Mikataba mingi iliyoridhiwa Kimataifa kwa manufaa ya wanawake wakiwepo Wanawake wa Tanzania; na kwa kuwa ni wanawake wachache sana wanaozielewa itifaki hizo; na kwa kuwa ni kwa manufaa yao; je, Serikali itakuwa tayari sasa kuweka utaratibu maalum ili wanawake waweze kuzielewa hizo itifaki zilizoridhiwa Kimataifa ikiwepo Tanzania?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu imeridhia itifaki mbalimbali na itifaki hizo zinatekelezwa katika stage mbalimbali kwa Wizara mbalimbali, masuala ya wanawake ni masuala mtambuka; hivyo basi, Wizara mbalimbali zinapotunga sera zao, zinafuatia yale ambayo yapo katika itifaki ambazo zipo.

SPIKA: Ahsante. Muda hautoshi, naomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 4

Kuelimisha Jamii Juu ya Katiba Mpya ya Nchi Kabla ya Kuunda Katiba Mpya

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA aliuliza:-

Je, kabla ya kuandikwa kwa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuelimisha umma wa Watanzania juu ya Katiba iliyopo kwanza kabla ya kuandika hiyo mpya ili Wananchi waweze kutoa michango mizuri ya usahihi ya kuboresha Katiba ya sasa na kuweza kupata Katiba Mpya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, imejipanga kikamilifu kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika kutekeleza azma hii ya Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria imepanga kutekeleza masuala yafuatayo:-

- (i) Kuhamasisha umma kuhusu mchakato wa Katiba Mpya na maudhui ya Katiba ya sasa kwa kuandaa matangazo kwenye TV, redio, magazeti na vipeperushi;
- (ii) Kuandaa vipindi vya majadiliano katika TV, redio kuhusu Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

- (iii) Kuchapisha nakala ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 kwa lengo la kuzisambaza kwa Wananchi na makundi mbalimbali na taasisi ili wajielimishe kuhusu maudhui ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, sanjari na juhudi hizi za Serikali, kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8 ya 2011, Tume ya Kuratibu na Kukusanya Maoni Kuhusu Katiba Mpya, ina dhima ya kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Ni imani ya Serikali kuwa, kupitia mkakati huu tuliojiwekea, Wananchi watapata fursa ya kuifahamu Katiba ya sasa na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kutoa maoni yao katika mchakato wa kupata Katiba Mpya.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tunafahamu kwamba Wananchi walio wengi hawaifahamu Katiba iliyopo; na kwa kuwa Serikali imetamka kwamba ipo tayari kutoa elimu na kuchapisha nakala 500,000 kwa ajili ya kuelimisha Wananchi. Je, Serikali inaweza kutuhakikishia kwamba zoezi hili la kuchapisha na kusambaza kwa Wananchi kwa ajili ya kutoa elimu litafanyika mapema kabla ya kufika Tume ili Wananchi waweze kujiweka tayari mapema hasa wale walioko vijijini?

SPIKA: Wewe unauliza swali moja tu maana siyo mwenye swali la asili.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa ndiyo inaandaa taratibu za kuchapisha. Kwa hiyo, tunategemea kwamba hata kabla Tume hajaanza, Wananchi watakuwa wameanza kupata vipeperushi ili kuweza kujielimisha. Vilevile Tume itaweka utaratibu utakaowezesha kutoa mafunzo kwa Wananchi kuelewa vizuri Katiba ya sasa ili iwe sehemu ya mjadala kwa ajili ya kupata Katiba Mpya.

Na. 5

Kuongezeka Kwa Idadi ya Watoto Yatima Wasio na Makazi Jijini Dar es Salaam

MHE. REBECCA M. MNGODO aliuliza:-

Idadi ya watoto yatima wasio na makazi wenye umri wa kuanza shule inazidi kuongezeka hasa Jijini Dar es Salaam na kwenye miji mingine nchini:-

Je, Serikali inalichukuliaje tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali, nakushukuru kwa kuniruhusu nitumie Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Wabunge Marafiki wa Twiga Stars, Timu ya Mpira wa Miguu ya Wanawake kwa kuichapa Namibia mabao matano; wanawake wanaweza, Twiga Stars wanaweza, Watanzania tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto yatima wanaoishi mitaani, kuombaomba na kufanya kazi kama kuosha vioo vya magari na kuuza bidhaa ndogo ndogo katika miji mikubwa nchini likiwemo Jiji la Dar es Salaam. Serikali haipendezwi na hali hii, kwa sababu pamoja na mambo mengine linawaweka watoto hawa katika mazingira hatari na kuwakosesha haki zao za msingi kama zilivyoinishwa katika Sera ya

Taifa ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, pamoja na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki za Watoto iliyosainiwa na kuridhiwa na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada mbalimbali kutatua tatizo la watoto yatima waishio mitaani ikiwemo kutunga Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, ambayo inaweka jukumu la kwanza la malezi ya mtoto kwa familia na jamii husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mtoto pia inaweka wajibu wa kulinda na kukuza haki za mtoto aliyepo katika eneo husika kwa Serikali za Mitaa. Kwa mujibu wa Sheria hii, Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuwa na orodha ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuwapa misaada, kuishi kwa staha ndani ya jamii na kuendeleza kwa kutumia rasilimali zilizopo.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa idadi ya watoto wa mitaani inaongezeka; na kwa kuwa ni haki yao ya msingi kupata elimu kufuatana na Malengo ya Maendeleo ya Milenia:-

(i) Je, Serikali inafanya nini ili hao watoto walioko mitaani nao wapate haki yao ya msingi ya elimu kwa sababu elimu kwa wote ndiyo Mpango wa Maendeleo wa Milenia?

(ii) Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali za Mitaa zina wajibu wa kuwa na orodha ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kuwapa misaada; je, ni misaada gani ambayo imeshatolewa kwa watoto hao ambao wanaishi katika mazingira magumu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, narudia kwenye Sheria ya Mtoto, kifungu cha 94(4), ambapo jukumu kubwa limewekwa kwa Serikali za Mitaa. Sisi Serikali Kuu, kazi yetu kubwa ni kutoa Sera na Miongozo kuhusu kushughulikia tatizo la watoto yatima likiwemo suala la kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge naye ni Diwani, nitamwomba atusaidie kulisitiza hili katika Vikao vya Halmashauri kwamba, tunawasaidia vipi watoto yatima ili nao waweze kupata elimu. Niseme pia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha wanatoa elimu ya ufundi kwa watoto wanaoishi mitaani.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali za Mitaa zinaonekana kushindwa kuwaratibu watoto hawa na kuwasaidia; na kwa kuwa tuna hakika kabisa Wananchi kama wangepata idadi kamili ya kuweza kujua watoto hawa wanaishi katika mazingira gani wangukuwa tayari kutoa misaada. Je, Serikali itatusaidiaje NGOs mbalimbali ambazo zimekwisharatibu majina hayo ya watoto na zipo tayari kuratibu kwa kutumia Sheria ya Watoto ili tuweze kuhakikisha tunaisaidia Serikali pamoja na Serikali za Mitaa kuhakikisha hao watoto wanapata huduma na haki zao za elimu pamoja na chakula?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza, ni suala zuri ambalo amelisema kwa sababu katika Halmashauri mbalimbali tayari uhakiki umefanyika. Sisi katika level ya Serikali Kuu, tulichokifanya tayari tumeunda kikosi kazi kinachojumuisha Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, UN Organisations na Mashirika mbalimbali kwa ajili ya kufanya utekelezaji kuhusu misaada mbalimbali kwa watoto wanaoishi mitaani. Tutaomba NGOs zilizopo zivasiliane na mwakilishi wao ambaye anaingia katika hicho kikosi kazi cha kuangalia ni jinsi gani tutatua tatizo hili la watoto yatima na watoto wengine wanaoishi katika mazingira magumu. Nakushukuru sana.

Na. 6

Njia ya Upatikanaji Maji – Igunga

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Asilimia 80 ya mazingira ya Jimbo la Igunga ni miamba ya Ziwa na sehemu kubwa ya Jimbo hilo ni mbuga kame isiyo na maji ardhini hivyo suluhisho la kudumu la kupata maji ni kuvuna maji ya mvua kwa kuchimba malambo/mabwawa makubwa kama yale ya Mwazungu na Bulenya:-

Je, kwa nini Serikali isichimbe mabawa makubwa mawili katika Jimbo la Igunga ili kuwaondolea Wananchi wa maeneo hayo ardha na kero wanayopata ya kukosa maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza Miradi kulingana na vipaumbele vya Halmashauri na Wananchi. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Vijiji vya Mwamashimba, Matinje, Makomero, Bulumbela, Bulungamilwa, Mwalala, Mwabakima, Mwamala, Isenengeja na Mwandihimiji, vimechaguliwa na Halmashauri kutekeleza awamu ya Kwanza ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, inahusisha vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Kati ya hivyo, Miradi kwa ajili ya vijiji vinne vya Mitanje, Bulumbela, Bulungamilwa na Mwandihimiji, imepata ridhaa ya kutangaza zabuni ya nje kumwajiri mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu kulingana na shilingi bilioni 1.3 zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012.

Katika vijiji hivyo vinne, Wananchi wamechagua teknolojia ya visima. Aidha, usanifu wa Miradi katika vijiji sita vilivyobaki bado unaendelea ambapo vijiji viwili vya Mwamashimba na Mwabakima vimechagua teknolojia ya mabwawa. Usanifu utakapokamilika na fedha kupatikana, Miradi hiyo itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuwa, yale maeneo ambayo hayana maji ardhini, suluhisho lake la kuvuna maji ya mvua. Naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kuingiza ujenzi wa mabwawa katika mipango yake kama ilivyofanya kwa Vijiji vya Mwamashimba na Mwabakima.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri yenye kuweka matumaini kwa Wananchi wa Igunga, lakini pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mkakati gani hasa Serikali inao kwa kujenga mabwawa makubwa katika Jimbo la Igunga ili kuwaondolea tatizo la maji Wananchi hawa ambalo ni kubwa sana kutokana na mazingira yao ya asili?

(ii) Kwa kuwa tatizo la maji Jimbo la Igunga ni kubwa sana; ni lini basi mpango wa kufikisha maji kutoka Ziwa Victoria utatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kafumu, kwa kuanza kuuliza maswali yanayohusu Idara ya Maji. Kuhusu mkakati wa Serikali wa kujenga mabwawa kwenye jibu la msingi, Halmashauri za Wilaya tumeomba ziweke kwenye mipango yake mabwawa yale madogo, lakini Serikali itashughulikia mabwawa makubwa, yale tunayoyaita *strategic dumps* ambayo yatakuwa yanahudumia maeneo makubwa. Kwa hiyo, mipango hii itakuwa imeandaliwa na Halmashauri za Wilaya, Serikali itapeleka utaalum wa kuweza kuwaelekeza namna gani miradi ya mabwawa iweze kujengwa.

Katika swali lake la pili kuhusu maji kutoka Ziwa Victoria, Serikali imeshaanza mchakato wa kupeleka maji Tabora, Nzega na Igunga, kwa kuanza na usanifu. Tumeshanza hadidu za rejea na kwa sababu miradi hii tunashirikiana pamoja na washirika wa maendeleo ni lazima tupate kibali cha Benki ya Dunia. Kwa hiyo, tumeshawasilisha hadidu za rejea za usanifu wa awali wa Miradi hii ili tuweze kupata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu, tuweze kujenga Mradi wa kupeleka maji Tabora, Nzega na Igunga.

MHE. SULEIMAN J. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mpango wa kuleta maji ya Ziwa Victoria, Jimbo la Kishapu ulikamilika kwa usanifu, uratibu, hadidi za rejea na michoro yote na tayari tunasubiri fedha ili maji yale yatoke Mji wa Shinyanga yapite Kata za Songwa, Modiruhumbo na Uchungu kuelekea Mji Mdogo wa Muhunze. Nini tamko la Serikali kwa sababu tunasubiri fedha, Wananchi wangu wanapata tabu ya maji tunataka tamko la Serikali ni lini maji hayo yatafika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli tumesema tutapeleka maji kutoka Kahama kwenda maeneo ya Kishapu, lakini kabla ya kufanya hivyo lazima uanze na usanifu na usanifu umekamilika lakini lazima uingize kwenye mpango wa kibajeti. Sasa hii yote tumeamua kufanya Awamu ya Pili ya Programu ya Sekta ya Maji katika kupeleka miji mingine ambayo maji yamefika Kahama.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuishukuru Wizara kwa juhudi zake za utafutaji wa maji katika Jimbo la Rombo. Kwa kuwa jitihada za kuchimba visima kwa ajili ya kutafuta maji kule Rombo zinaelekea kukwama kutokana na maji kukosekana ardhini. Je, Wizara ipo tayari kutoa ruhusa sasa zile fedha ambazo zinatumiwa kwa ajili ya uchimbaji wa visima ambavyo hata hivyo vimeshindwa kuzaa matunda zitumike kwa ajili ya kutengeneza malambo ili kukinga maji kwa manufaa ya watu wa kule Rombo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya maeneo ambayo wameamua kuchimba visima, yameshindikana kupatikana maji na tunasema katika Sera yetu ya Maji kwamba, lazima uwashirikishe Wananchi kwenye Miradi hii kwa sababu kuna gharama za utekelezaji. Sasa kitakachotakiwa kufanyika hapa ni kwamba, Wananchi pamoja na yule msimamizi, waamue badala ya kuchimba visima sasa wajenge bwawa. Serikali itakuwa tayari kuruhusu kazi hiyo iweze kufanyika.

Na. 7

Mpango wa Ukarabati wa Miradi ya Maji ya Kitaifa

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Ilani ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015 inatamka wazi juu ya mpango wa ukarabati wa Miradi ya Maji ya Kitaifa ikiwemo Mradi wa *Makonde Water Supply Authority*:-

Je, utekelezaji wa ukarabati wa Mradi wa Maji wa Makonde umefikia hatua gani hadi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mipango ya muda mfupi ya kukarabati Mradi wa Maji wa Makonde, Serikali ilitenga shilingi bilioni 1.2 kati ya mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2010/2011 zilizopelekwa kwa Mhandisi Mkazi wa Mradi huo. Fedha hizo zilitumiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kanunua bomba kuu kati ya Mitema, Kitangari na Nanyamba lenye kipenyo cha inchi 12 na urefu wa kilomita 8.8 na mabomba mengine na viungo vyake kwa ajili ya matanki matatu yaliyopo Chiwambo yenye vipenyo kati ya inchi 6 hadi 10 yenye jumla ya kilomita 66;
- (ii) Kununua pampu nne za kusukuma maji, mbili kwa kituo cha Mkunya zenye uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 100 kwa saa kila moja na nyingine mbili kwa Kituo cha Makote zenye uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 80 kwa saa kila moja;
- (iii) Kununua pampu moja na mota kwa ajili ya kusukuma maji katika Kituo cha Mahuta yenye uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 40 kwa saa;

- (iv) Ufungaji wa *transformer* eneo la Kitangari;
- (v) Ukarabati wa vyanzo vya maji vya Mkunya na Kitangari;
- (vi) Ununuzi wa mabomba kwa ajili ya Mikumbi, Chilangala, Bahati na Vijiji vya Wilaya ya Newala; na
- (vii) Kununua na kufunga dira za maji 1,000.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka huu wa Fedha wa 2011/2012, imetenga shilingi milioni 334 ambazo tayari zimepelekwa kwa Mhandisi Mkazi wa Mradi. Fedha hizo zitatumika kukamilisha ukarabati wa Kituo cha Kusukuma Maji katika eneo la Makote na kukiwezesha chanzo cha maji cha Mkunya kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 1,100 hadi 2,000 kwa siku. Kazi hiyo itakamilika mwezi Machi, 2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mipango ya muda mfupi, Serikali tayari imeanza kutekeleza mpango wa muda mrefu wa ukarabati wa Mradi wa Makonde. Upembuzi yakinifu ulikamilika mwezi Agosti 2011 na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya usanifu wa kina, uandaaji wa vitabu vya zabuni na ujenzi wa Mradi.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati wa muda mfupi na ukarabati wa muda mrefu unaotarajiwa kufanyika, lakini kwa sasa eneo hili la Makonde kwa maana ya Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijini, lina matatizo makubwa ya maji. Mahitaji kwa siku ni mita za ujazo milioni 12, lakini zinapatikana asilimia 42 tu ya mahitaji hayo yanayotakiwa. Wakati mambo hayo yanaendelea, lipo jambo ambalo likifanyika linaweza kusaidia sana kupunguza tatizo hili nalo ni kufanya ukarabati wa chujio lililopo Kitangari. Chujio lile kwa sasa linapitisha maji ujazo wa mita milioni tatu, lakini likikarabatiwa lina uwezo wa kuchuja maji mita za ujazo milioni tisa kwa siku, jambo ambalo lingepunguza tatizo:-

(i) Serikali haioni haja ya kufanya marekebisho haya ili tupunguze tatizo lililopo kwa Wananchi wetu wa Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini?

(ii) Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alifanya ziara Mkoani Mtwara Julai mwaka jana. Kwenye Mkutano wa Viongozi alioufanyia kwenye Makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Newala aliahidi kutoa shilingi milioni tatu kwa ajili ya kusaidia tatizo la maji Mtwara Vijijini kwa maana ya Tarafa ya Nanyamba na Tandahimba. Hadi hapa ninapongea, fedha hizo hazijafikishwa kwa ajili ya kutatua tatizo hili. Nini ahadi ya Serikali kukamilisha jambo hili haraka na hasa Watendaji wa Wizara?

SPIKA: Umesema shilingi milioni tatu au milioni mia tatu?

MHE. JUMA A. NJWAYO: Milioni mia tatu.

SPIKA: Maana nilishangaa, milioni tatu ni kidogo mno. Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli kama anavyosema, kuna haja ya kukarabati chujio ambalo linaweza kuongeza uzalishaji wa maji ya eneo lile. Nakubaliana naye na katika mipango yetu kazi hiyo itafanyika.

Kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais, niseme tu kwamba, kwa kuwa Rais ameahidi, maana Serikali ya CCM ndiyo itatekeleza, kwa hiyo, naomba usiwe na wasiwasi, ahadi ya Rais itatekelezwa kama alivyoahidi.

Na. 8

Uharibifu wa Wanyama – Hifadhi ya Burigi

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA aliuliza:-

- (a) Je, ni Wananchi wangapi wanapakana na Hifadhi ya Burigi waliowahi kulipwa fidia kutokana na wanyama waharibifu wa mazao kama Tembo, Nyati na kadhhalika?
- (b) Je, ni kiasi gani cha fidia kimelipwa tangu mwaka 2000 hadi 2011?
- (c) Je, ni huduma gani za jamii wamesaidia katika maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara imewalipa jumla ya Wananchi saba fedha za kifuta machozi kwa madhara waliyoyapata kutokana na wanyamapori wakali katika Wilaya za Ngara na Karagwe. Jumla ya shilingi 250,000 zililipwa mwaka 2005/2006. Fedha hizi zililipwa kwa familia za marehemu wanne waliouawa na Tembo na Wananchi watatu waliojeruhiwa. Aidha, kwa mwaka 2011, Wizara imelipa jumla ya shilingi 12,400,000 kwa Wananchi 124 walioharibiwa mazao yao na wanyamapori katika Wilaya zinazozunguka Hifadhi hiyo. Fedha hizo zimelipwa baada ya jumla ya ekari 290.75 kuharibiwa na wanyama waharibifu.
- (b) Jumla ya shilingi 12,650,000 zililipwa kwa ajili ya kifuta machozi na jasho kwa Wananchi waliopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Fedha zililipwa kwa watu kutoka Wilaya za Karagwe na Ngara.
- (c) Wizara hutoa fedha kiasi cha asilimia 25 zinazotokana na mapato ya uwindaji wa kitalii katika Pori la Akiba la Burigi/Biharamulo pamoja na Pori la Kimisi. Fedha hizi hutolewa kila mwaka, ambapo hupelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya husika kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2001 hadi 2011, jumla ya shilingi 22,349,000 zilipelekwa kwenye Wilaya zinazozunguka mapori hayo kwa ajili ya maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kipindi cha mwaka 2005/2006, Kampuni ya Uwindaji wa Kitalii ya *Kilimanjaro Game Trails*, ilichangia shilingi milioni moja na laki tano kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika Kijiji cha Ruhuta. Aidha, mwaka 2007 Kampuni hiyo ilichangia Dola za Kimarekani 1,000 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Kijiji cha Ruhuta. Pia Wizara inaendelea na ujenzi wa kituo cha askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika Kata ya Nyakakika Wilayani Karagwe ili kuwapunguzia Wananchi athari wanazopata kutokana na wanyamapori waharibifu.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nitoe kilio cha Wananchi wa Biharamulo Magharibi kwamba swali lao la msingi halijapata majibu, inaonekana wamejibiwa watu wa Ngara na watu wa Karagwe. Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutoa majibu yanayostahili kwa Wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

SPIKA: Yatakuwa matatu hayo, wewe uliza moja labda.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Ahsante. Kwa kuwa sasa kumekuwepo kero ya askari wanyamapori ambao wanakwenda kuchukua mifugo ya Wananchi kutoka kwenye eneo la kufugia, maeneo sahihi ya Vijiji na kuwaingiza kwenye eneo la Hifadhi na kuwatoza pesa ambazo hazitolewi risiti; je, Serikali inasemaje juu ya bughudha hii kwa Wananchi? Naomba kauli ya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, moja; swali la msingi lilivyokuja kwetu Wizarani liliulizia fidia kwa Wananchi wanaozunguka Pori hilo bila kutaja kwa uhakika kwamba kinachotakiwa ni kwa wale wa Biharamulo. Kwa Biharamulo niseme tu kwamba, walinufaika na wao kama nilivyosema hasa kwa asilimia hii 25 inayokwenda, maana kwa mwaka 2009 tu Wananchi wa Biharamulo kama sehemu ya asilimia hii 25 walipata jumla ya shilingi 2,080,000 kama mgao wao wa sehemu ya fedha inayokwenda kule. Kwa mwaka jana pia walipata shilingi 1,970,000, lakini kama nilivyosema, mgao huu umekuwa ukienda kwa Vijiji vyote vinavyozunguka Pori husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili; Serikali itazingatia maana ni kweli kwamba kumekuwepo na uharibifu mkubwa unaosababishwa na mifugo katika Hifadhi ya Pori hilo. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Wizara, kwanza, atoe taarifa za uhalali ili Wizara iweze kuchukua hatua husika. Pili, tushirikiane kuwaelimisha wafugaji waliovamia Pori hilo kwa upande wa Biharamulo kwamba hilo ni eneo la Hifadhi na siyo malisho ya mifugo.

Na. 9

Mgogoro wa TANAPA na Vijiji Vinavyozunguka Hifadhi

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

Kumekuwepo na mgogoro kati ya TANAPA na Vijiji vinavyozunguka Hifadhi kama vile Kata ya Pahi, Kinyasi, Kwadelo, Kisese na Itaswi:-

Je, ni lini Serikali itatoa ufumbuzi wa kudumu juu ya mgogoro huo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vilivyotajwa havipakani na Hifadhi yoyote iliyoko chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), bali vinapakana na Pori la Akiba liliulikanalo kama Pori la Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Mkungunero lilitangazwa rasmi kuwa Pori la Akiba kwa Tangazo la Serikali (GN) Na. 307 la tarehe 18 Oktoba, 1996. Pori hili lina ukubwa wa kilomita za mraba 627.95. Sehemu kubwa ya Pori hili ipo katika Wilaya ya Kondo, Mkoani Dodoma. Pori hili linapakana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kwa upande wa Kaskazini, upande wa Kusini linapakana na Vijiji vya Indiri, Ihari, Kwadelo na Mlongia. Kwa upande wa Mashariki, linapakana na Kijiji cha Kimotorok katika Wilaya ya Simanjiro. Pia kwa upande wa Kaskazini Mashariki limepakana na Kijiji cha Irkiushbor Wilayani Kiteto. Kwa upande wa Kusini Mashariki na upande wa Magharibi, linapakana na Vijiji vya Itaswi, Maumo, Isongolo, Ikengwa na Keikei. Pori hili ni muhimu sana hasa kwa uhai wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire maana ndiyo chanzo cha maji cha Mto Tarangire.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Pori la Akiba la Mkungunero limekuwa na mgogoro na Vijiji vinavyopakana na Pori hili. Wizara ya Maliasili na Utalii, imechukua hatua mbalimbali za kutatua mgogoro huu, hatua ambazo kwa kiwango kikubwa zinaonekana kuzaa matunda.

Katika kufanya kazi ya usuluhishi, Wizara imekutana na wakazi wanaoishi kandokando ya maeneo hayo. Imekutana pia na Uongozi wa Mkoa wa Manyara pamoja na Uongozi wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo katika Pori hili kwa wenyeji wanaoishi kandokando, kuingiza mifugo, lakini pia kufanya makazi, kulima, kuchunga mifugo na kukata miti ndani ya Pori la Akiba, kitu ambacho ni kinyume cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, hasa vifungu vya 15(1) na (2).

Mheshimiwa Spika, Wizara, kama nilivyosema, imekutana na uongozi husika kwenye Mikoa ya Dodoma na Manyara na kujadili na kupata mwafaka wa pamoja kuhusu migogoro na kikao hiki kilifanyika tarehe 19 Januari, 2009. Kumekuwepo na vikao mbalimbali vya ujirani mwema kati ya Uongozi wa Pori la Akiba la Mkungunero na Viongozi wa Wilaya ya Kiteto, Simanjiro na Kondoa na kuzungumzia ajenda ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, nia pia imekuwepo ya kufanya vikao zaidi katika ngazi ya Vijiji ili kuanza kubainisha matatizo na kuyatatua yote kwa pamoja. Aidha, mwezi Agosti 2011, Waziri katika kuwasilisha bajeti ya Wizara hapa, aliahidi kuunda Timu Maalum ya Kitaifa, itakayohusisha wataalam kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Vijiji ili kupitia upya mipaka inayoleta migogoro katika maeneo haya. Timu hiyo imeshaundwa na itaanza kufanya kazi wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa pia limeanzisha Kitengo Maalum kwa ajili ya kushughulikia migogoro inayokuwepo kati ya mipaka na Hifadhi. Tutaendelea kutoa fursa za kuzungumza na kuelimishana na jamii ambazo ni jirani na Pori hili na imani yangu ni kuwa, kwa njia ya mazungumzo na kuelimishana, mwafaka wa kudumu wa mgogoro huu utapatikana.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa amesema timu hiyo imekwishaundwa; je, imeshaanza kazi?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema watafanya mazungumzo na Wananchi ili kuwaelimisha. Je, kazi hiyo imeshaanza na kama bado ni lini mtaanza kuwaelimisha Wananchi hao?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Timu imeshaundwa, hadidu za rejea zimeshaandaliwa na Programu ya Kazi tayari imeandaliwa. Timu hii imeshaanza kazi hasa kwa kuwezesha zaidi na TANAPA katika maeneo yale yanayopakana na Hifadhi. Kwa upande wa Mapori ya Akiba kama hili la Mkungunero, hii Timu haijafika, lakini mara tu rasilimali zitakapopatikana, Timu hii itafika na kati ya maeneo ambayo Timu itafika kwa uhakika ni pamoja na eneo hilo la Mkungunero. Elimu imeshaanza kutolewa na kila taasisi pamoja na mamlaka inayohusika. Kwa upande wa Hifadhi za Taifa (TANAPA) imeanza na kwa upande pia wa Mapori haya ya Akiba, Idara inayohusika na Mapori yenyewe pia imeshaanza kutoa elimu hii kwa Wananchi wanaozunguka maeneo haya.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya swali la msingi ambapo amenukuu kwamba Pori la Akiba la Mkungunero lilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 307, ambalo ni kweli; na kwa kuwa katika tangazo hilo ilibainishwa wazi kwamba Pori hilo la Akiba litakuwa ndani ya Wilaya ya Kondoa; na kwamba mgogoro sasa upo kati ya Pori hilo na Vijiji vya Wilaya ya Kiteto na Wilaya ya Simanjiro kwa maana ya Kijiji cha Kimotorok na Kijiji cha Irkiushbor, kwa maana hiyo imevuka mpaka wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Kondoa.

Je, Serikali haioni kwamba ndiyo chanzo cha tatizo hili kwa kukiuka Tangazo la Serikali lililoanzisha Pori hilo kwa kuvuka mipaka ya Kondo kuingia katika Wilaya zingine na Mikoa mingine kinyume na tangazo lenyewe na kwamba kuna haja ya kusahihisha haraka hili?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, baada ya uhakiki kufanywa na timu ya Wizara mwaka jana, wamebaini kwa uhakika kwamba, Pori la Mkungunero haligusi Kijiji cha Kimotorok kilichoko Simanjiro. Kwa hiyo, kwa sasa kwa taratibu na kwa mitazamo ya Wizara, Kimotorok haipo kwenye Mkungunero. Kumekuwepo na pendekezo la kupanua Pori hili, lakini pendekezo hilo lililetwa na watu wa Idara husika na kujaribu kuchukua jumla ya hekta 5050 kutoka Kimotorok na kuchukua pia hekta 5050 kutoka Irkiushbor.

Mapendekezo haya yalikalaliwa na wenyeji na sasa kilichoamuliwa na Wizara ni kwamba, eneo walilopendekeza la heka 5050 kutoka Kijiji cha Irkiushbor litakuwa kwenye utaratibu wa Programu ya WMA ya Endema ambayo imeendelezwa na Wananchi wa Vijiji hivyo husika, lakini Kimotorok haipo kabisa katika Mkungunero.

Na. 10

Hitaji la Huduma ya Simu za Mkononi – Kata za Sanza na Iseke

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI aliuliza:-

Katika Tarafa ya Nkonko Wilayani Manyoni kuna minara miwili tu ya simu; mmoja wa Vodacom na wa pili wa Airtel, lakini Wananchi wengi wa Tarafa hiyo hasa Kata za Sanza na Iseke wanakosa kabisa mawasiliano. Je, ni lini kampuni za simu zitapeleka huduma ya simu za mkononi katika Kata za Sanza na Iseke?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya Vodacom tayari imekwishafanya utafiti ili kuboresha huduma za mawasiliano ziweze kufika katika maeneo yote yenye usikivu hafifu na yale ambayo hayajafikiwa kabisa na huduma hiyo hususan maeneo kama vile ya Kata za Sanza na Iseke. Kampuni hiyo iko katika hatua za maandalizi ya kutekeleza azma yake ya kuongeza usikivu kwa maeneo yasiyo na usikivu, matarajio ni kwamba ifikapo Aprili, 2012 watakuwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya Airtel kwa uapnde wake imekwishafanya utafiti wa kitaalam katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge na tayari maeneo hayo yamewekwa katika orodha ya maeneo yaliyo katika mpango wa kufikisha huduma za mawasiliano katika mwaka huu wa fedha.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya kutia moyo. Hata hivyo, nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Mheshimiwa Rais Kikwete, alipotembelea Kata za Sanza na Iseke, alitoa ahadi thabiti kwamba, maeneo haya yatapata mawasiliano, ahadi ambayo mpaka sasa haijatekelezwa. Aidha, Kampuni ya Airtel imefika katika Kata za Sanza, wamefanya utafiti kama alivyosema Naibu Waziri; sawa sawa, wamechagua mpaka eneo la kujenga mnara, lakini Airtel wamechelewa utekelezaji kwa kipindi cha miezi sita. Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari sasa kuwasukuma Airtel waje wajenge mnara katika eneo ambalo walishachagua na kuingia mkataba na mkulima?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais ni agizo na Rais akishaagiza, sisi tunatekeleza. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli

kwamba Kampuni ya *Airtel* imeshafika pale kuangalia na kuchagua eneo na kama nilivyojibu katika swali la msingi vilevile Kampuni ya *Vodacom* nayo imefanya utafiti. Uwekaji wa minara unachukua mchakato mrefu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba taratibu zote za kisheria zinafuatwa, ikiwa ni kuangalia vilevile hali ya mazingira kama iko salama ili waweze kuhakikisha kwamba mnara unapokuwa pale, hauleti madhara yoyote ya kijamii.

Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira, Kampuni ya *Airtel* iko mbioni na tutahakikisha kwamba tunashirikiana nayo ili kuhakikisha tunawawekea mnara Wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu la nyongeza linafanana na swali lililoulizwa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kuna Kata nne ambazo tayari nilishawasilisha maombi Ofisi ya Waziri kwa ajili ya kushughulikiwa na ahadi ilishatolewa. Vijiji hivyo ni vya Kata ya Wasa, Kata ya Maboga, Kata ya Lumuli na Kata ya Mugama. Kata hizi zina matatizo makubwa ya mawasiliano ambapo ningependa nipate majibu ya ratiba ya utekelezaji wa Kampuni hizo kama ahadi ya Waziri alivyokuwa ameahidi kwamba Kampuni hizo zimeshajawekea utaratibu zitafika na sisi Wabunge tsubiri na mimi bado nasubiri. Ninachoomba ni ratiba na ninapowasiliana na wananchi wenzangu waweze kuona nazungumzia kitu ambacho kinatekelezeka ki-*timetable*.

SPIKA: Sawa, Waziri naomba ujibu *timetable* kwa yote.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Dokta Mgimwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi wa saba wakati Wizara yetu inawasilisha bajeti yake, tuliwaomba Wabunge wote watoe maeneo ambayo hayafikiwi au hayana mtandao; tumefanya hiyo kazi na sasa hivi tupo katika mchakato wa *tender* lakini kabla hatujakwenda mbali zaidi, Wizara yangu katika Bunge la Mwezi wa Nne itakuja na wataalam tena ili waweze kukutana na Wabunge kuonesha ratiba kama ambavyo Dokta Mgimwa ameuliza.

Na. 11

Uhitaji wa Mawasiliano ya Simu – Manda Ludewa

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA) aliuliza:-

Eneo la Manda Ludewa lina matatizo mengi ya mawasiliano ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka haraka mawasiliano ya simu katika eneo la mwambao wa Kata za Ludewa eneo la Ikuwo na Makete?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Tknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa mawasiliano hafifu yanayopatikana katika maeneo mengi nchini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kijiografia, kibiashara na kiuchumi, ikichangiwa pia na changamoto kubwa ya upatikanaji wa nishati muhimu kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi kwa pamoja ni kubwa, hasa ukizingatia hali ya kiuchumi ya Wananchi, Makampuni ya Mawasiliano pamoja na Serikali kwa ujumla. Aidha, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma ya mawasiliano inapatikana kwa Wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo changamoto hizo, Wizara yangu kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tayari imechukua jitihada za makusudi kwa kushirikiana na Sekta Binafasi, Wahisani katika Sekta ya Mawasiliano na Makampuni ya Simu ili kuhakikisha upungufu huo unaondolewa. Aidha, mnamo mwezi Julai, 2011, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCAF), uliorodhesha maeneo yote yanayohitaji mawasiliano kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuanza upembuzi na hatimaye kupeleka huduma husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mchakato huo umeanza kwa kutangaza zabuni mnamo mwezi wa Septemba, 2011 ambapo kampuni mbalimbali za mawasiliano tayari zimewasilisha maombi kwa ajili ya kufanyiwa tathmini. Kazi ya utekelezaji wa zoezi la kupeleka mawasiliano litafanyika kwa awamu hususan baada ya kukamilisha utaratibu wa manunuzi na hatimaye kupata kampuni zitakazofaa kwa kazi hii, ambapo katika awamu ya kwanza ya utekelezaji huo, utagusa maeneo ya Mwambao wa Ziwa Nyasa yakiwemo maeneo ya Manda, Ludewa, Ikuwo na Makete yamejumuishwa kama ambavyo nimesema.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa zoezi la kupeleka mawasiliano katika maeneo yaliyoorodheshwa itatolewa rasmi kwa Waheshimiwa Wabunge katika Vikao vya Bunge la mwezi Aprili 2012.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yanakosa huduma za simu kule Ludewa ni mengi hasa maeneo yote ya Mwambao wa Ziwa Nyasa zikiwemo Kata za milimani ambako ni Kata ya Lupanga pamoja na Madilu, Kata ya Makonde, Lupingu, Lifuma, Kilondo pamoja na Lumbila:-

- (a) Tunaomba kujua utekelezaji utakuwaje kwenye maeneo hayo?
- (b) Kuna baadhi ya maeneo minara ya simu ipo kwa mfano Ludewa Mjini, Mlangali na Lugalawa, simu ya mteja *network* imejaa, lakini Wananchi wakipiga simu haziendi, wakipiga simu mara nyingine wanaongea nusu dakika simu inakatika lakini huku inakatwa na kuzima au mara nyingine simu imejaa *network* siku mbili mawasiliano ya simu inakuwa hakuna au mara nyingine *network* imejaa na hasa Vodacom lakini *Data Three G* zinakuwa hakuna. Waziri kwa kufanya hivyo huoni kwamba hawa Vodacom wanajivunja heshima wao wenyewe pamoja na Wizara yako? Naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILINO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoainisha katika jibu langu la msingi, utekelezaji unakwenda kulingana na mpango ambao tumejijwekea. Kwa sababu tunatambua na Serikali yetu hii ni sikivu na shirikishi, tumesema mwezi wa nne tutakuja tuongee na Wabunge tukubaliane kwamba sisi kama Wizara katika mpango wetu wa UCAF tumepanga kufanya hivi. Wabunge watakuwa na nafasi ya kutoa michango yao waweze kueleza kwamba, mlivyopanga hivi kutokana na mahitaji ya Wananchi katika Jimbo langu ingefaa iwe hivi na hivi na hii nadhani itatusaidia sote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ambayo tayari yana mnara lakini kuna msongamano, nimhakikishie tu Mbunge kwamba, katika zoezi hili vilevile tunaangalia uwezekano wa kuongeza *capacity* katika maeneo ambayo tayari yana msongamano. Nitafurahi zaidi kama nitapata takwimu za kutosha kutoka kwa Wabunge kwa maeneo ambayo yana matatizo kama alivyosema Mbunge.

SPIKA: Ahsante. Muda wenyewe umekwisha, twende Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Felix Mkosamali, atauliza swali hilo.

Na. 12

Umeme – Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Mpango wa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo ulitarajiwa kukamilika mwezi Novemba 2010 lakini hadi sasa zoezi hilo halijakamilika; na kwa kuwa taarifa ya mkandarasi husika ni kuwa baadhi ya sehemu kama Biturana hazitaweza kufikishiwa umeme kwa mujibu wa ramani yake:-

- (a) Je, ni lini sasa zoezi la kuweka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo litakamilika?
- (b) Je, kwa nini Mkandarasi ameshindwa kufikisha umeme maeneo yote ya Kibondo Mjini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zoezi la kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo limekamilika kwa asilimia tisini, ambapo tayari wateja 1,046 wamekwishaunganishiwa huduma ya umeme. Mradi huu unatekelezwa na mkandarasi aitwaye *Namis Corporate Ltd.* na unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 33 umbali wa kilomita 20, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 0.4 kilomita 48, ufungaji wa *transformer* 20 na uunganishaji umeme wa wateja waliokadiriwa awali 1,368.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizokwishaanyika hadi sasa ni pamoja na upimaji na usanifu wa njia za umeme, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 33 ambao umekamilika kwa asilimia mia moja pamoja na ufungaji wa transfoma umekamilika kwa asilimia mia moja. Aidha, katika Mradi huu, kipaumbele kiliwekwa kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya kama Sera ya Taifa ya Nishati inavyosema, baada ya hapo mipango ya kupeleka umeme maeneo mengine ya Wilaya ya Kibondo itakamilika kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida utekelezaji wa kazi hutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za utekelezaji wa Mradi husika na makubaliano ya Kimkataba yaliyofikiwa na pande zote husika. Kiasi cha fedha za utekelezaji ambao Mradi ulipatiwa hakitoshi kufikisha umeme maeneo yote ya Wilaya ya Kibondo. Kipaumbele ilikuwa ni kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo yaliyokubalika na baada ya hapo maeneo mengine yatapatiwa umeme kutegemeana na upatikanaji wa fedha za utekelezaji.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Maeneo muhimu kama Hospitali ya Wilaya ya Kibondo, Magereza na vitongoji vyenye watu wengi kama Vitongoji vya Kumeruro, kwa Manyanya, Kumwayi, ambavyo ni maeneo ya Kibondo Mjini havijapata umeme na watu wengi wamekuwa wakiomba kupatiwa umeme lakini hawapati huduma hiyo; kwa nini maeneo muhimu kama haya hayajapata umeme?
- (b) Licha ya umeme kufika vijijini na mijini lakini kumekuwa na ongezeko la gharama za umeme na Serikali inataka kuongeza bei ya umeme. Je, Serikali imezingatia hali halisi ya maisha ya Watanzania katika kuongeza bei ya umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, katika maeneo aliyoyataja nimepata wasiwasi kidogo aliposema kwamba, hospitali haijapatiwa umeme na hili tutakwenda kulifanyia kazi, kwa sababu katika utaratibu wa Mradi ambao ulikuwepo wa kupeleka umeme Kibondo, tunajua kwamba kutoka kwenye *power house* mpaka Kibondo Makao Makuu kwa DC

Mjini ni kama kilomita 4.3 na pana *line branch off* pale inakwenda mpaka Magereza kama kilomita saba. Kwa hiyo, hilo lipo na lipo kwenye utaratibu.

Yapo maeneo mengine ambayo yamepatiwa umeme, hili la Biturana kwa mujibu wa maelezo tuliyokuwa nayo, Biturana ni kijiji tofauti, kipo pale pale karibu na Kibondo lakini ni kijiji tofauti. Kipo kama kilomita tano au sita kutokea Makao Makuu ya DC.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, Biturana na hayo maeneo mengine unayoyasema, yatafanyiwa tathmini kulingana na mahitaji yake ya umeme yaliyokuwepo na yatapatiwa umeme. Kipaumbele ilikuwa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na maeneo yanayozunguka, tukitoka hapo kipaumbele cha pili ni kwenda Kakonko Wilaya mpya kule kwa Mheshimiwa Obama.

Mheshimiwa Spika, hivyo ndiyo vipaumbele tulivyojiwekea, kwa hiyo, naomba nimshauri Mbunge kwamba kama yapo maeneo ambayo unadhani yanastahili lakini hayapo, njoo tuyatathmini tuwape REA kazi hiyo wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili la ongezeko la bei ya umeme, naomba niseme tu kwamba, tulishasema awali kwamba ongezeko la bei ya umeme kwa muda huu ambao kwenye Gridi ya Taifa tunazalisha umeme mwingi kwa kutumia mafuta ya *diesel*, ambayo kupanda kwake ni *sporadic* yanapanda, yanashuka na yanapanda sana, hatuwezi kutegemea kwamba tutabaki na gharama zile zile za uzalishaji. Kwa hiyo, tulichosema ni kwamba hadi hapo ambapo tutaingiza vyanzo vingine ambavyo ni nafuu zaidi; gesi, makaa ya mawe na kadhalika, ambalo jambo hilo kwa upande wa gesi linatarajiwa kuingia katika kipindi cha miezi minane hadi mwaka kutegemeana na ukamilishaji wa bomba la mafuta, tutapunguza gharama za umeme, kulingana na umeme unaozalishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme wazi ijulikane kwamba, hili ongezeko la bei linakwenda kwa sababu hakuna namna ya kufanya, ongezeko lililolombwa ni asilimia 150, kwa wateja tumepeleka asilimia 40 na Serikali ikabeba mzigo mwingine.

SPIKA: Tuendeleo na swali linalofuata, Waheshimiwa muda ni kama mnavyoona, Mheshimiwa Amina Abdulla Amour.

Na. 13

Kufutwa kwa Ushuru kwa Mafuta ya Taa.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR Aliuliza:-

Ingawa lengo la kufutwa ushuru wa mafuta ya taa ni kuwawezesha Wananchi wengi vijijini kumudu kununua mafuta hayo kwa matumizi yao mbalimbali; badala yake mafuta hayo yamekuwa hayaonekani vijijini na imefahamika kuwa yanachakachuliwa na *diesel* na kuuzwa kama *diesel*:-

Je, ni mafanikio gani yamepatikana baada ya Serikali kuchukua hatua za kudhibiti uchakachujaji huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali mafuta ya taa yalikuwa yanatozwa kodi kiasi cha shilingi hamsini na mbili kwa lita. Hata hivyo, ili kukabiliana na tatizo la uchakachujaji, mwezi Julai 2011, Serikali ilifanya uamuzi wa kupandisha ushuru kwenye mafuta ya taa mpaka kufikia shilingi mia nne na senti thelathini kwa lita. Uamuzi huo umeiwezesha EWURA kuidhibiti biashara hiyo haramu nchini. Takwimu zinaonesha kuwa, tatizo la uchakachuzi kwa sasa limepungua kutoka asilimia karibu sabini na nane mwaka 2007 hadi kufikia takribani asilimia kumi mwishoni mwa Disemba 2011.

Mheshimiwa Spika, baada ya juhudi za kukomesha mafuta ya taa kutumika katika kufanya uchakuchuzi, mauzo ya mafuta ya *diesel* na *petrol* yameongezeka katika kipindi cha miezi ya sita ya kwanza ya mwaka 2011. Kiasi cha mauzo ya *petrol* kilikuwa takriban lita milioni mia mbili na sabini na *diesel* lita milioni mia nne na kumi na tatu. Baada ya mabadiliko ya ongezeko la ushuru kwenye mafuta ya taa sambamba na kuanzishwa kwa programu ya kuweka vinasaba, kuanzia Julai mpaka Disemba 2011, kiasi cha mafuta ya *petrol* na *diesel* yaliyouzwa kuanzia Julai hadi Disemba kimefikia lita mia tatu na tano milioni kwa *petrol* na lita milioni mia tano na kumi na saba, ambalo ni ongezeko kama la milioni mia moja na tano kwa *diesel*.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi huo, mauzo ya ndani ya mafuta ya taa kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba 2011 yamepungua ikilinganishwa na mauzo ya mwezi Januari hadi Juni 2011 kutoka lita milioni mia moja na sita hadi lita milioni sitini, hali ambayo inadhihirisha kwamba, matumizi makubwa ya mafuta ya taa awali yalikuwa kwenye uchakachujaji. Hata hivyo, pamoja na kwamba mauzo ya mafuta ya taa yamepungua, makusanyo ya kodi za Serikali yatokanayo na ushuru wa mafuta ya taa yameongezeka ukilinganisha na miezi sita ya mwanzo. Hivyo, ongezeko la ushuru kwenye mafuta ya taa limesaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la uchakachujaji wa mafuta.

Serikali kupitia *EWURA* itaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa ubora wa mafuta na kuhakikisha kuwa mafuta ya taa yanayoagizwa, yanatumika kwa njia iliyokusudiwa na hayachanganywi na *diesel* na *petrol* kwa maana hiyo. Juhudi hizi zina lengo la kuhakikisha kuwa, kila aina ya mafuta yanapatikana katika maeneo yote hapa nchini kwa ubora unaoastahili.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa athari ya uchakachujaji hupoteza Pato la Taifa, uharibifu wa magari pamoja na uharibifu wa biashara ya nje na ndani; na katika jibu alilolitoa Waziri amekiri kuwa uchakachujaji ulikuwepo:-

- (a) Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuleta mapendekezo ya kutoa adhabu kali sana kwa wale wachakachujaji?
- (b) Faida za hatua hizi ilikuwa ziwafikie Wananchi; je, Serikali imefanya tathmini baada ya kuongezeka kodi ya mafuta imekuwaje? Naomba nipatiwe jawabu.

SPIKA: Ahsante. Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana tupo nje ya wakati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni lazima niseme kwa hii asilimia kumi iliyobaki sasa, hawa wamekuwa wachakachuzi sugu. Kwa hiyo, katika hali hii, ndani ya Bunge hili kuanzia kwenye Kamati ya Nishati na Madini mpaka humu ndani, suala la adhabu kali limezungumzwa sana. Niseme tu kwa niaba ya Serikali kwamba, tumeshawaambia *EWURA* wanalifanyia kazi, litakwenda kwenye Kamati ya Nishati na Madini, yaje mapendekezo ya adhabu kali kwa sababu bado inaonekana kuna hawa wachakachuzi sugu ambao ni kama asilimia kumi, kumi na tano iliyobaki. Kwa adhabu za sasa hivi; milioni saba, milioni kumi na milioni kumi na tano kwa vituo na haya maghala, inaoonekana haitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli kabisa kwamba, kwa hawa sugu inabidi tuweke adhabu kali na mapendekezo tutayaleta Bungeni katika vikao vinavyofuata.

Mheshimiwa Spika, hili lingine ni kweli kwamba, mafuta ya taa ule ushuru umeongezeka kidogo, mwanzoni makusanyo yote ya mauzo yalikuwa kama milioni mia tisa na sitini na nane na sasa hivi kwa ongezeko hili pamoja na kwamba mafuta ya taa yameshuka lakini bado tunaona kuna ongezeko kama la bilioni 4.1 kwa Shilingi za Tanzania kwa makusanyo miezi hii sita ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, pesa hizi zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na zikifika huko Wizara ya Fedha ndiyo wanazipangia matumizi. Mapendekezo ya awali yalikuwa kwamba, pesa hizi zitoke na kwa sababu zinatoka kwenye nishati zirudi kwenye Wakala wa Nishati Vijijini ili kuboresha maendeleo na upatikanaji wa nishati ya uhakika katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mapendekezo ya Bunge yalikuwa hayo na Serikali tunayafanyia kazi kwa hayo makusanyo yanayopatikana.

Na. 14

Ufufuaji wa Viwanda Nchini

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE aliuliza:-

Serikali ina lengo la kuboresha mikakati ya kukuza ajira nchini ili watu wengi hususan vijana waweze kupata ajira:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna ulazima wa kufufua viwanda kama vile Viwanda vya Nguo, Chuma na vinginevyo ili viweze kutoa ajira kwa vijana?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge wote na Watendaji wetu wa Bunge, kwa sara zenu ambazo zimefanikisha matibabu yangu kule India. Napenda vilevile kutumia fursa hii, kwa kutumia Bunge lako Tukufu, kuwashukuru Watanzania wote wakiwemo na wale wa Moshi Vijijini, kwa kuniombea sana hadi nimepona. Kama ninavyoonekana, nimepona naendelea vizuri, lakini jitihada za kuongeza mtori ziko pale pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali ina lengo la kuboresha mikakati ya kukuza ajira nchini ili watu wengi hususan vijana waweze kupata ajira. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imefanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa, viwanda mbalimbali vilivyokuwa vya umma vinafufuliwa ili viweze kutoa ajira kwa vijana na kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kubinafsisha viwanda ili sekta binafsi iweze kuchangia katika kuvifufua na kuviendeleza.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Programu hii yamekuwa mazuri kwa ujumla kwani kati ya viwanda 15 vya nguo vya umma, viwanda 12 viliweza kufufuliwa na kufanya kazi, ikilinganishwa na kiwanda kimoja tu kilichokuwa kikifanya kazi mwaka 1997. Aidha, kwa sasa kuna viwanda vya nguo 13 vinavyofanya kazi na vinatoa ajira kwa wafanyakazi takriban 22,000 ikilinganishwa na wafanyakazi 14,226 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda vya chuma, viwanda vinne vinaendelea kufanya kazi kati ya viwanda kumi vilivyokuwa vya umma. Aidha, viwanda vipya 17 vya chuma vimeanzishwa na hivyo kufanya idadi ya viwanda 21 na kutoa ajira ya wafanyakazi 5000. Vilevile kumekuwa na ongezeko la viwanda vya sekta nyingine vilivyobinafsishwa kama vile saruji, vinywaji, sabuni na pia kusindika nafaka vimeimarishwa na vinaendelea vizuri na uzalishaji na vinatoa ajira. Pamoja na ufufuaji wa viwanda vilivyokuwepo, Serikali imeendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vipya ikiwa ni pamoja na vile vya EPZ, Viwanda vya Chuma vikiwemo M. M. *Integrated Steel Mills, Aluminium Africa Limited, Iron and Steel Company, Trishallah Steel Mill, Kamal Steel Mills, Nyakato Steel Mills, Steel Master Company* na *Jeje Industries*. Aidha, Miradi ya Mkaa wa Mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Chuma cha Liganga, inayotekelezwa kwa ubia kati ya Kampuni Sichon Hongdo ya China na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ni sehemu muhimu ya kuinua viwanda mama vya chuma nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa viwanda ambavyo wawekezaji wameshindwa kuvifufua na kuviendeleza, mazungumzo yanaendelea kati ya Shirika Hodhi la Taifa (*Consolidated Holding Corporation*) na wamiliki wa viwanda hivyo kulingana na mikakati ya mauzo ili kukubaliana upya utaratibu wa kuvifufua na kuviendeleza ili kuzalisha ajira zaidi.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, je, Bunge lako Tukufu linaweza likapewa taarifa kuhusu urejeshwaji wa Mgodhi wa Kiwira?
- (b) Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala la viwanda vya chuma; amesema katika jibu lake la msingi kwamba kuna viwanda kumi vilivyoweza kubinafsishwa lakini kati ya viwanda hivyo, vinne vinaendelea kufanya kazi. Je, ni kwa kiwango gani viwanda hivyo vinaendelea kufanya kazi na pia nini hatma au tamko la Serikali kuhusiana na hivyo viwanda vingine sita? Ahsante.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Pedenciana Kikwembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za kurejesha Mgodhi wa Kiwira zinafanywa na Wizara ya Nishati na Madini na nafikiri nitawasiliana na wenzangu wa madini na nishati na nitakapopata jibu la uhakika kabisa kwamba imefikia hatua gani, basi nitampa Mheshimiwa Kikwembe na hata ikibidi Bunge lako Tukufu litaarifiwa kwamba utaratibu umefikia wapi.

Kuhusu viwanda kumi vya chuma vilivyokuwa vinafanya kazi lakini vine tu ndiyo vinafanya kazi, siyo jambo la ajabu kwa viwanda vilivyokuwa vinafanya vizuri miaka ya 1970, 1980 leo kuwa havifanya kazi vizuri. Jambo la maana ambalo limefanyika ni hili ambalo nimelisema; kwanza, tunaangalia Mikataba ambayo ilisainiwa kati ya PSRC na wale ambao walipewa vile viwanda na anayefanya tathmini hiyo ni *Consolidated Holding Corporation (CHC)*. Tunaangalia ni vipengele vipi ambavyo vimekiukwa ili kuona utaratibu wa kuvirudisha katika Serikali ili wapewe watu wengine ambao wanaweza wakafanya kazi vizuri zaidi. Nimezungumza pia hapa jinsi ambavyo viwanda vingine vipya vimeibuka kutokana na upatikanaji wa *raw material*, labda masoko yamekuwa mazuri, teknolojia tofauti na ambayo ilikuwepo, vyote vinachangia kufanya watu waache kuzalisha katika kiwanda fulani cha zamani na kuanzisha viwanda vipya. Hivi 17 ni dalili nzuri kwamba tunakwenda vizuri na tuna viwanda 21 vya chuma ukiunganisha na hivyo kumi, lakini jitihada ziko pale kuhakikisha kwamba hivyo sita ambavyo havifanyi kazi hapa kama vinaweza vikafanya kazi basi inafanyika na tutaendelea kufanya hivyo na kuliarifu Bunge lako kadiri hatua zinavyokuwa zinafanikiwa.

Na. 15

Uhitaji wa Vituo vya Polisi

MHE. AGNESS E. HOKORORO aliluliza:-

Kutokana na kukosekana kwa Vituo vya Polisi kwenye Wilaya za Mtwara kumesababisha matatizo ya jinsi ya kuwahudumia mahabusu yakiwemo ya mshtaki kumpelekea chakula mshtakiwa na baadhi ya Wananchi kukosa uwezo wa kutoa huduma kwa mahabusu na gharama za mgambo:-

- (a) Je, Serikali itakuwa tayari kuunga mkono nguvu za Wananchi wanapojitolea kujenga Kituo cha Polisi?
- (b) Kwa nini Serikali isichukue hatua za makusudi za kuanzisha *Operation* Maalum ya ujenzi wa Vituo vya Polisi sanjari na ulinzi shirikishi kwa lengo la kupunguza uhalifu na kuleta amani miongoni mwa raia?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Agness Hokororo, kwa ridhaa yako, naomba nirejee katika swali namba moja ambapo Mheshimiwa kidawa aliuliza swali la nyongeza kuhusu mbwa aliyekufa Zanzibar. Jibu ni kwamba, Serikali tuna habari na jambo hilo na kwa kweli linafanyiwa kazi na hivi sasa tuko katika utaratibu wa kuweza kupata mbwa ambao watafanya kazi hizo. Niseme tu kwamba, kwa sasa hivi hao mbwa wapo katika mazoezi na mafunzo, kwa sababu siyo mbwa wa kawaida na hili suala analifuatilia kwa karibu sana Kamishna Mussa Ali Mussa na anayo majibu yote lakini nimhakikishie Mbunge kwamba, hilo linafanyiwa kazi.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kuunga mkono jitihada za Wananchi katika ujenzi wa Vituo vya Polisi. Hata hivyo, kabla ya kuanza ujenzi, Wananchi wamshirikishe Mkuu wa Polisi wa Wilaya husika (OCD) ili kupata ushauri wa kitaalam.
- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga Vituo vya Polisi katika Wilaya na Kata zote hapa nchini. Kazi hiyo, inafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kupitia Mpango wa Ulinzi Shirikishi, Serikali inaendelea kuhamasisha Wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuimarisha amani na usalama katika maeneo yao, hii ikiwa ni pamoja na kuchangia katika ujenzi wa Vituo vya Polisi na ununuzi wa vitendea kazi.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa mshtaki kumhudumia mshtakiwa siyo sahihi kwa kuwa unawanyima haki Wananchi na kuwapelekea kutokuripoti vitendo viovu kwa kuogopa kuhudumia na kuwaongezea gharama zaidi?

SPIKA: Hukumuelewa swali aulize tena?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agness Hokororo na kama nimelielewa swali vizuri, nafikiri anazungumzia juu ya kuhudumia mahabusu. Niseme kwamba, imekuwa ni utaratibu na utamaduni ambao umekuwepo muda mrefu sana na sasa tupo katika mchakato ama katika kipindi ambacho tunazama utaratibu mzima wa mahabusu zinavyokwenda kuhusu watu ambao wapo mahabusu lakini bado kesi zao hazijafikia kufanyiwa uamuzi.

Kwa hiyo, niseme kwamba ni suala ambalo bado tunalishughulikia, tunalitazama upande wetu sisi na upande wa Mahakama kuona ni utaratibu gani ambao unafaa. Hiki ni kitu ambacho kimekuwepo kwa muda mrefu, lakini kuwepo kwa muda siyo kwamba ni sahihi ama siyo sahihi, lakini ni jambo ambalo tunalitazama upya. Mheshimiwa Mbunge, ningekuomba uwe na subira kidogo wakati tunatafuta jibu katika suala hilo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na umepita sana. Sina taarifa ya wageni isipokuwa nina matangazo yafuatayo kwamba:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba, leo tarehe 31 Januari, 2012 baada ya kuahirisha Bunge, kutakuwa na Kikao cha Kamati, Ukumbi Namba 227, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala. Huo muda itakuwa vigumu kwa sababu mimi mwenyewe ninatangaza kwamba Wenyeviti wote wa Kamati mbalimbali za Bunge, yaani Kamati ya Uongozi, kutakuwa na kikao leo Jumanne, tarehe 31, saa tano asubuhi

katika Ukumbi wa Spika. Labda hii ya Mheshimiwa Pindi Chana, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati hiyo waende Chumba Namba 227 baada ya kipindi cha maswali.

Halafu nina tangazo lingine; Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Wabunge wa Chama hicho leo tarehe 31 Januari, 2012 katika Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Wao watakaa saa nane. Baada ya hapo, Katibu karibu kwa hatua inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania wa Mwaka 2011 *(The Tanzania Livestock Research Institute Bill, 2011)*.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, 2011)*.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu wa Mwaka 2012 *(The Anti-money Laundering (Amendments) Bill, 2012)*.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 *(The Constitutional Review Amendments Bill, 2011)*.

(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Kanuni ya 93(2)(a), naomba kutoa hoja kwamba, Miswada ifuatayo iliyokwishasomwa kwa Mara ya Kwanza, ishughulikiwe katika hatua zaidi ya moja. Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka, 2011 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, 2011)*, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu wa Mwaka 2012 *(The Anti-Money Laundering (Amendments) Bill, 2012)*, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 *(The Constitutional Review Amendments Bill, 2011)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Bunge liliridhia Miswada iliyotajwa hapo juu ipitie katika hatua zake zote)

SPIKA: Kwa hiyo, Miswada iliyotajwa itapitia katika hatua zake zote katika Bunge hili kufuatana na Kanuni ya 93(2).

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 47 ambayo inaruhusu Bunge kujadili jambo lolote la dharura ambalo limepotokea hapa nchini siku hiyo au siku za karibuni, nilikuwa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipate Taarifa ya Serikali kuhusiana na mgomo wa madaktari unaoendelea na Taarifa hiyo ijadiliwe hapa Bungeni. Sote ni mashahidi kwamba, hivi sasa hali ya Wananchi ni mbaya sana, vifo kwenye hospitali zetu vimeongezeka na madaktari ambao wametii amri ya Waziri jana kwenda kwenye vituo vyao vya kazi, wamesaini tu na kuweka vifaa vyao chini. Kwa hiyo, kuna mgomo baridi na hali hii ni mbaya sana na sisi kama Bunge hatuwezi kuendelea kufanya shughuli nyingine yoyote na kuacha kulizungumzia suala hili.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali itupe Taarifa Rasmi kuhusu hili na Bunge liweze kujadili na kuweza kuona hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa kwa ajili ya kuweza kutatua hali hii nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Siwaulizi kama imeungwa mkono au vipi kwa sababu tayari nimepewa taarifa na Serikali kuanzia jana kwamba, inatoa kauli kuhusu jambo hili kutokana uamuzi wa Waziri Mkuu na mengine yatakayoendelea leo. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, taarifa ya Serikali itatolewa halafu kama lazima tujadiliane hapo ndiyo tutaangalia kuhusu taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana ni kwamba, baada ya Kipindi cha Maswali, Kikao cha Bunge kinaahirishwa mpaka kesho asubuhi ili kutoa nafasi; kwanza, kwa Kamati ya Uongozi, kukaa lakini pia kutoa nafasi kwa Kamati mbalimbali zinazopaswa kushughulikia Miswada inayohusika, waweze kuikamilisha vizuri. Tunatambua kwamba, wiki mbili tulizokuwa nazo Dar es Salaam zilikuwa kidogo za msukosuko, Kamati nyingi hazikuweza kukamilisha mambo yao. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.12 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 1 Februari, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*